**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA ( OR – TAMISEMI)**

SIMU……………………………………………. **SHULE YA SEKONDARI MANDWANGA**

**S.L.P 55**

**MTAMA – LINDI**

**TAREHE ……………………………..**

**Kumb Na. A.1 / MSS / S.1910 / VOL 14**

**MWANAFUNZI…………………………………………………………..**

**S.L.P…………………………………………………………………….**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MANDWANGA**

**1:0** Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii. Hii ni bahati ambayo wengi wameitamani na wameikosa, hivyo hongera sana. Unatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa

Shule ya sekondari MANDWANGA ipo katika kijiji cha Mandwanga, kata ya Mandwanga, tarafa ya Nyangamara, wilaya ya Mtama.

Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe……………………… unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe…………………………na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe………………………….. usiporipoti mpaka tarehe hiyo itakuwa umepoteza sifa ya kujiunga na shule hii.

**2:0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2:1 SARE YA SHULE**

(a) Sare ya shule hii kwa wavulana ni suruali ndefu mbili (2) rangi ya khaki kwa mshono unaokubalika
na shati mbili (2) nyeupe (tetroni) mikono mifupi na tai ya khaki.
Kwa wasichana sketi mbili (2) rangi ya kijani za kuvuka magoti na nusu kanzu mbili (2) nyeupe za mikono mirefu kwa wale wanaovaa hijabu, kwa wasio vaa hijabu mashati mawili (2) rangi nyeupe yenye mikono mifupi.
Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na viatu vyeusi vya kufunika miguu vyenye visigino vifupi.

(b) Hijabu inaruhusiwa kwa wasichana. Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule.

(c) Kila mwanafunzi aje na track suti za bluu bahari na raba kwa ajili ya michezo na T-shirt, T- shirt zinapatikana hapa shuleni kwa bei ya TSH. 12,000/=

**2:2 MICHANGO YA SHULE**

Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni kama ifuatavyo:

a. Tshs 5000/= kwa mwezi kwa wanafunzi wa kutwa kwa ajili ya manunuzi ya sukari, chumvi, vifaa vya jikoni na kuwalipa wapishi.
b. Tshs 10,000/= kwa mwezi kwa wanafunzi wa kambi kwa ajili ya manunuzi ya sukari, chumvi, vifaa vya jikoni na kuwalipa wapishi.
c. Unga au mahindi kilo 50 kwa muhula kwa wanafunzi wa kambi.
d. Unga au mahindi kilo 25 kwa muhula kwa wanafunzi wa kutwa.
e. Mboga kilo 30 kwa muhula kwa wanafunzi wa kambi.
f. Mchele kilo 18 kwa muhula kwa wanafunzi wa kambi.
g. Mboga kilo 15 kwa muhula kwa wanafunzi wa kutwa.
h. Unatakiwa kuja na Rimu moja ya karatasi na siyo pesa

**2:3 VIFAA VYA USAFI**

Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo:-

a. Panga, Jembe na Fyekeo kwa ajili ya usafi wa mazingira ya shule.
b. Ndoo ndogo kwa ajili ya kazi za shule.

**3:0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

**3:1** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

(a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni jambo la lazima.
(c) Kutimiza kwa makini kazi za masomo nje ya darasa ( homework).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na kuwajibika ipasavyo.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuizingatia kikamilifu wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

**3:4 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi.
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.
5. Kupigana na kupiga

6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma au kuchochea na kuongoza au kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Mwanafunzi kuwa na simu.

**4:0 MAMBO MENGINE MUHIMU.**

(a) Mwanafunzi apimwe afya yake kwenye hospitali ya Serikali na kujaziwa fomu (medical examination form) iliyoambatanishwa.
(b) Fomu ya mzazi / mlezi kukiri itajazwa siku ya mwanafunzi kuripoti shuleni.
(c) Mwanafunzi aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa au hati ya kiapo cha mahakama ( Affidavit) endapo hana cheti hicho.
(d) Gharama ya matibabu ya mtoto ni mzazi au mlezi husika.

**5:0** Kila mzazi / mlezi na mwanafunzi asome kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Aidha fomu zilizoambatanishwa zijazwe kikamilifu na kuwasilishwa shuleni siku ya kuripoti.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**THEONEST JOSEPH MANJWANGA**

…………………………………………

**MKUU WA SHULE**

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL GOVERNMENTS**

**MANDWANGA SECONDARY SCHOOL**
**P.O BOX 55**
**MTAMA – LINDI**
**Date…………………**

Ref. No……………………………………………….
To the Medical Offficer
………………………………………………………………

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MS…………………………………………………..**

Please examine the above named student and give us report regarding his / her suitability for secondary school studies.

1. Stundent's full name……………………………………………………………………
2. Blood…………………………………………………………………………………………….
3. Stool…………………………………………………………………………………………….
4. T.B test………………………………………………………………………………………….
5. Syphilis test……………………………………………………………………………………..
6. Urine examination……………………………………………………………………………..
7. Eye test………………………………………………………………………………………….
8. Chest……………………………………………………………………………………………..
9. Ears………………………………………………………………………………………………..
10. Spleen…………………………………………………………………………………………….
11. Abdomen……………………………………………………………………………………….
12. Pregnancy (Girls only)……………………………………………………………………

I certify that above student is suitable / unsuitable for studies. Give reasons………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………

Name of medical officer……………………………………… Signature………………………………..

Date……………………………………… Stamp……………………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR – TAMISEMI)**

**SHULE YA SEKONDARI MANDWANGA**

…………………………………………

…………………………………………

…………………………………………

Tarehe………………………………..

Mkuu wa shule

Shule ya sekondari Mandwanga

S . L. P 55

MTAMA – LINDI

**YAH: KUKUBALI / KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA KIDATO CHA…………………… MWAKA……………….**

Nakutaarifu kuwa nimepokea barua yako Kumb Na………………………………………………………………………..

Ya tarehe……………………………………. Nimesoma yote uliyonitumia na ninakuarifu kuwa NINAKUBALI / SIKUBALI nafasi hiyo. Nipo tayari kufuata kanuni na taratibu za shule kama zilivyoainishwa kwenye sheria za shule.

Ninatumia juhudi na maarifa yangu katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

………………………………………………………………….. ……………………………………………………………………….

Jina na sahihi ya mwanafunzi Jina na sahihi ya mzazi / mlezi

Tarehe………………….. Tarehe………………………………

Futa isiyohusika.

**UTHIBITISHO WA MZAZI / MLEZI**

**KUHUSU TABIA NA MWENENDO WA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………………………………………………nakubali mwanangu ndugu…………………………………………………………………asome katika shule ya sekondari Mandwaga kuanzia tarehe……….mwezi…………mwaka…………. Ninaahidi kwamba nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuhakikisha kwamba anatii sheria, kanuni na taratibu zote za shule wakati wote atakapokua masomoni hapo shuleni. Pale atakaposhindwa kuzitii sheria, kanuni na taratibu za shule hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

Anuani ya mzazi / mlezi…………………………………………………………………….

Sahihi ya mzazi / mlezi……………………………………………………………………..

Tarehe…………………………………………………………….

**UTHIBITISHO WA MZAZI / MLEZI**

**KUHUSU TABIA NA MWENENDO WA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………………………………………………nakubali nisome katika shule ya sekondari Mandwaga kuanzia tarehe……….mwezi…………mwaka…………. Ninaahidi kwamba nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuhakikisha kwamba natii sheria, kanuni na taratibu zote za shule wakati wote nitakapokua masomoni hapo shuleni. Pale nitakaposhindwa kuzitii sheria, kanuni na taratibu za shule hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………….

Sahihi ya mwanafunzi……………………………………………………………………..

Tarehe…………………………………………………………….